

HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA
[Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji]

Telegrams: "MSW"
Telephone: +0282750271
Fax: + 0282750376
E-mail: ded@maswadc.go.tz



S.L.P. 170,
MASWA.

Kumb. Na. MDC/ADM/F. II/51

24/03/2022

TANGAZO LA KAZI YA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa anawatangazia wananchi wote wenye sifa zilizoainishwa kwenye Tangazo hilo kuomba nafasi za kazi ya Mkataba wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri katika Mji wa Maswa na Malampaka.

Wakusanyaji wa mapato (Nafasi 4).

Majukumu ya kazi:-

1. Kukusanya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kutumia mashine za Kielectronic za kukusanyia mapato (POS).
2. Kuhakikisha fedha iliyokusanywa kupelekwa benki kwa wakati.
3. Kuhakikisha mapato yote yanayopaswa kukusanywa na Halmashauri na yanakusanywa kwa usahihi.

Sifa:

Waombaji wawe wenye Elimu ya Kidato cha nne na kuendelea ambao wana uelewa wa kutumia simu za tachi, sababu mapato yote ya Serikali yanakusanywa kwa kutumia mashine za Ki-electronic za kukusanyia mapato (POS) ambayo ina application sawa na simu za tachi.

Masharti ya waombaji katika kazi hii.


1. Awe raia wa Tanzania, umri kati ya miaka 21 hadi 45.

2. Waombaji wote wawe wameambatanisha cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha NIDA.
3. Waombaji waaambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detached CV) yenye anwani na namba ya simu za kuaminika pamoja na majina matatu ya wadhamini (referees) na anuani zao za kudumu ambapo wadhamini wawe na mali zisizohamishika.
4. Maombi yaambatane pamoja na nakala ya vyeti vyote vya kitaaluma vya waombaji.
5. Awe tayari kupangiwa kituo chochote cha kukusanya mapato (Maswa mjini au Malampaka).
6. Awe mwaminifu na mwadilifu katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kuhakikisha fedha za Serikali hazipotei.
7. Awe tayari kupokea na kufuata atakayopangiwa na Mkuu wake pasipo kuvunja taratibu na kanuni za fedha.

• **BARUA ZOTE ZITUMWE KUPITIA ANUANI**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA,
S.L.P. 170,
MASWA.**

- Pia barua zipelekwe masjala ya wazi ya Halmashauri ya Wilaya Maswa kuanzia tarehe 24/03/2022 na mwisho wa kupokea maombi tarehe 01/04/2022 saa 9:30.



Vivian M. Christian
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MASWA**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA**